

**NAIBU WAZIRI NDEJEMBI AONYA VITENDO VYA RUSHWA KWA
WATUMISHI WA IDARA YA ARDHI MKURANGA**

Na. Veronica Mwafisi-Mkuranga

Tarehe 28 Disemba, 2021

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deogratius Ndejembu ameonya vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Akizungumza na Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga katika kikao kazi chake na watumishi hao, Mhe. Ndejembu amewataka kujirekebisha na kufanya kazi kwa uadilifu na weledi ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima inayosababishwa na utendaji kazi wao usioridhisha.

Ameongeza kuwa, watumishi wa Idara hiyo ya ardhi wakiendelea na utamaduni wa kufanya kazi kwa kuweka maslahi binafsi mbele wataipotezea Serikali mapato na kuwanyima haki wananchi wa Mkuranga kupata maendeleo yanayotokana na kodi itayokusanywa na Serikali katika Halmashauri hiyo.

Akisisitiza uadilifu kwa watumishi hao, Mhe. Ndejembu amewataka wabadilike kwa sababu wamekuwa wakilalamikiwa kuwaonea wananchi kwa kuwaomba rushwa na kutowashauri vizuri kwenye masuala yanayohusu umiliki wa ardhi.

“Nimeambiwa hapa Mkuranga hata mimi nikihitaji shamba natakiwa kuwa na kitu kidogo cha kuwapatia watumishi wa Idara ya ardhi ambao wameweka maslahi yao binafsi mbele, na wala sitaki kumtaja mtu mmoja mmoja hapa zaidi ya kuwasisitiza mbadilike”, Mhe. Ndejembu amefafanua.

Kuhusiana na migogoro inayoibuka, Mhe. Ndejembu amewataka Watumishi wa Idara hiyo kuwa watatuzi wa migogoro badala ya kuwa chanzo cha migogoro.

Mhe. Mhe. Ndejembu amefanya ziara ya kikazi ya siku moja katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma wa Halmashauri hiyo, ikiwa ni pamoja na kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini unaoratibiwa na Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).